**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 1 No. 1 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i1.92


# Matumizi ya Misimu Moingoni mwa Wanafunzi: Uchunguzi Kifani katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Editha Adolph**
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Tanzania

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2022-12-28*
*Rekebishwa: 2023-03-12*
*Kubalika: 2023-04-28*
*Chapishwa: 2023-05-19*

***Maneno Muhimu***
Misimu
Wanachuo
Dar es Salaam
Vipera vya misimu

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Adolph, E., (2023). Vyanzo vya Misimu kwa Wanafunzi katika Kiswahili. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *1*(1), pp. 9-17.

*Copyright © 2023*
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Mtafiti wa makala hii anachunguza vyanzo vya misimu kwa wanafunzi katika Kiswahili. Mtafiti ametumia mbinu za hojaji, usaili na uchambuzi wa matini katika suala zima la kutimiza malengo ya makala hii. Kwa kutumia mbinu ya hojaji, mtafiti aligawa hojaji 15 kwa wanachuo 15 wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mtafiti pia kwa kutumia mbinu ya usaili, alifanya mahojiano ya ana kwa ana kwa watafitiwa wake ili kupata data stahiki. Aidha, mtafiti alisoma nyaraka zinazohusiana na mada husika kama vile: majarida, kamusi, tasinifu, vitabu mbalimbali na kadhalika. Kwa pamoja mbinu hizi zimekamilishana katika kumpatia mtafiti data faafu na hivyo kutimiza malengo ya makala hii. Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo ya Fishman (1972). Data ya makala hii imechambuliwa kwa kutumia mkabala wa maelezo. Matokeo ya makala hii yamebainisha kuwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na kutumia msamiati sanifu pia hutumia misimu kutoka katika nyanja tofautitofauti katika mawasiliano yao ya kila siku. Mtafiti amechunguza misimu inayotokana na uwanja wa utani, soka na sanaa. Makala hii ni muhimu kwa wanaisimu kwani inabainisha misimu mbalimbali inayotumiwa na wanachuo wa chuo husika hususan kutoka nyanja za utani, soka na sanaa. Hii itatoa msukumo kwa wasanifishaji wa lugha ya Kiswahili kusanifisha misimu husika. Inapendekezwa kuwa watafiti wa lugha wachunguze misimu inayotokana na mitandao ya kijamii, aina mbalimbali za misimu, misimu inayotumika katika maeneo mbalimbali kama vile shuleni, vijiweni, hospitalini, ofini na kadhalika. Aidha, tafiti fuatizi zifanyike kuhusiana na vyanzo vingine vya misimu tofauti na vile vilivyoangaziwa katika makala hii, kwa mfano, ufanyike utafiti juu ya misimu itokanayo na michezo, siasa, milipuko ya magonjwa, matukio mbalimbali yanayojitokeza katika jamii, ndoa na kadhalika.

## Utangulizi

Misimu imekuwa ikipewa nafasi katika jamii pamoja na ukweli kuwa ni maneno yanayozuka na mengine kupotea. Hii ni kutokana na masuala mbalimbali yanayojitokeza katika jamii tuishimo. Masuala hayo ni pamoja na: matukio kadha wa kadha, mlipuko wa magonjwa mbalimbali, siasa, sanaa, ukuaji wa sayansi na teknolojia, utani, siri, soka miongoni mwa machache. Yote hayo huwapa watumiaji wa lugha raghba ya kujiundia msamiati unaoweza kukidhi haja ya mawasiliano miongoni mwao. Msamiati huu ndiyo ujulikanao kama misimu kwani ni maneno yasiyisanifishwa na mingine huzuka tu na kutoweka ilhali mengine yakishika mizizi na kusanifishwa. Misimu imefasiliwa na wataalamu mbalimbali miongoni mwao ni: (Mulokozi, 1996; Chapman, 1995; Msanjila, 2009; King'ei, 2010) kwa pamoja wanadai kuwa misimu ni lugha ya siri inayozungumzwa na kueleweka na kundi la watu wenye utamaduni mmoja kwa lengo la kujitenga na kundi kubwa la jamii husika.

Misimu ni kipera kimojawapo cha semi. Mulokozi (1989) anathibitisha usemi huu kwa kuainisha vipera vitano vya semi ambavyo ni vitendawili, methali, misimu, kauli-tauria, mafumbo na lakabu. Wamitila (2003) naye anaainisha vipera vya semi kama ifuatavyo: methali, mafumbo, vitendawili, nahau, misimu na misemo. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa utanzu wa semi umeundwa na vipera vya nahau, methali, vitendawili, misemo, misimu, mafumbo, mizungu na lakabu. Vipera vyote vya semi hutumika kwenye jamii katika miktadha mbalimbali na vyote hubeba dhima tofautitofauti kwa kutegemea kusudio la mtumiaji. King'ei (2010) anaona kuwa misimu ni tatizo kwani huvunja kanuni za lugha sanifu kwa sababu si kila mtu huweza kufahamu maana iliyokusudiwa ya maneno hayo ya misimu kwa kuwa maana zake siyo za jumla kwa watumiaji wote wa lugha husika. Shayo (2015) alishughulikia semi zilizoandikwa katika maeneo ya biashara kama vile: hoteli, maduka, sokoni, migahawa, vibandani na magengeni. Katika utafiti wake aliangazia asili, muundo, miktadha na dhima za misimu aliyoishughulikia. Utafiti wa Shayo imetusaidia kubaini misimu mbalimbali hususan iliyoandikwa katika maeneo mbalimbali ya biashara kama ilivyobainishwa hapo juu, chimbuko na matumizi ya misimu hiyo. Hata hivyo, utafiti wa Shayo (2015) haukushughulikia vyanzo vya misimu kwa wanafunzi katika Kiswahili. Utafiti wa sasa unashughulikia suala hilo. Uchambuzi wa data ya makala hii umefanikiwa baada ya kutumia nadharia ambayo mtafiti ameitolea ufafanuzi katika kipengele kinachofuatia.

## Kiunzi cha Nadharia

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp 2006 nadharia ni muundo wa kidhanifu ambao huongoza utafiti katika mpangilio au utaratibu wa kukusanya na kuchanganua data katika hali ambayo inalenga kufikia malengo ya utafiti. Mtafiti wa makala hii ametimiza malengo yake ya kiutafiti kwa kuongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo ya Fishman (1972). Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo ni nadharia inayozingatia matumizi ya lugha kwa kutumia misingi kama vile: kutaka kujua nani anatumia lugha? Anatumia lugha ipi? Anaitumia na nani na kwa kusudi gani? Kutokana na misingi hii ya Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo tunaweza kubaini ni kundi gani hapo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam linapenda kutumia misimu na ni misimu ipi? Wanachuo hao wanatumia misimu hiyo na nani? Kwa nini wanatumia misimu hiyo katika

mawasiliano yao ya kila siku? Mbali na Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo kuasisiwa na Fishman (1972), ilishughulikiwa pia na Mekacha (1993), Msanjila (1999) na Chacha (2001).

Kutokana na Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo tumepata mwongozo kuwa watumiaji wa lugha wana tabia ya kuchagua lugha fulani na kuitumia katika eneo fulani. Kwa kawaida tabia ya watu ya kupenda kutumia lugha fulani katika eneo fulani hufungamana na amali na utamaduni wa jamii husika. Hali hii ya kiutamaduni hujengwa na kudumishwa na watu wa jamii moja, wenye utamaduni unaofanana na vilevile huwa na lugha moja inayowaunganisha. Hivyo, msingi huu umemwongoza mtafiti wa makala hii kujua ya kuwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam huchagua misimu na kuitumia katika mawasiliano yao ya kila siku katika maeneo ya chuoni. Pia imemuongoza kutambua ya kuwa hali hii inatokana na kufungamana kwa amali na utamaduni wa wanachuo hao. Aidha, hali hii ya kiutamaduni imejengwa na kudumishwa na wanachuo hawa wenye utamaduni unaofanana na kuwaunganisha. Mtafiti amewashirikisha watumiaji wa lugha husika ili apate taarifa za kuaminika na zenye uhakika kuhusiana na vyanzo vya misimu kwa watafitiwa hao anavyovifanyia utafiti. Aidha, nadharia hii imetuongoza katika suala zima la kubaini ni kundi gani la jamii linapenda kutumia misimu zaidi ya kundi jingine kwa kuzingatia kigezo cha rika katika jamii husika. Mbali na kiunzi hiki cha nadharia kilichotumika katika uchanganuzi wa data yetu, zipo mbinu mbalimbali zilizotuongoza kupata data hiyo. Mbinu hizo zinafafanuliwa hapa chini.

**Methodolojia**

Kipengele hiki kinahusu mbinu za utafiti zilizotumika katika ukusanyaji data ya makala hii na uchambuzi wa data hiyo. Ili kufikia malengo aliyojiwekea, mtafiti ametumia mbinu kadhaa za ukusanyaji wa data na uchambuzi wake. Lengo la kutumia mbinu zaidi ya moja ni kuziwezesha mbinu hizo kukamilishana na kuthibitisha uhakika wa taarifa zilizotolewa na watafitiwa wa makala hii. Mtafiti alitumia mkabala wa uwandani na chanzo cha maktabani. Kwa mujibu wa Neuman (1991) mkabala wa uwandani ni ule unaotumika katika ukusanyaji data kutoka kwa watafitiwa wengi kwa kutumia mbinu za hojaji na usaili kutoka kwa sampuli lengwa. Mkabala huu wa uwandani ndiyo uliyomwezesha mtafiti wa makala hii kukusanya data nyingi na kufanya majumuisho ya matokeo ya makala hii. Kutokana na mkabala wa uwandani, mtafiti alitumia mbinu ya hojaji na usaili. Hojaji ni njia rahisi ya kukusanya taarifa kutoka kwa watafitiwa wengi kwa mara moja na huokoa muda kwani haitumii muda mrefu na hutunza siri za watafitiwa. Kwa kutumia mbinu ya hojaji, data ilikusanywa na majumuisho yalifanywa kutokana na matokeo ya data husika. Mtafiti aligawa hojaji 15 kwa wanachuo 15 wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Aidha, mtafiti alikusanya data kupitia mbinu ya usaili ambayo ni mbinu ya ukusanyaji wa taarifa inayohusisha uulizaji wa maswali kwa njia ya mdomo, majadiliano, majibizano ya ana kwa ana au kwa njia ya simu lengo likiwa kukusanya taarifa na maoni kutoka kwa watafitiwa kuhusiana na suala la kiutafiti. Aidha, lengo la kutumia mbinu hii pia ni kulinganisha na kuchunguza mlingano wa data iliyokusanywa kwa kutumia mbinu ya hojaji. Mbinu ya usaili pia ilisaidia kupata maoni na mtazamo wa watafitiwa kuhusu vyanzo vya misimu kwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa upande wa chanzo cha maktaba, mtafiti alifanya uchambuzi wa matini kwa kusoma nyaraka mbalimbali mathalani: majarida, tasinifu na kadhalika. Baada ya kuona mbinu za utafiti wetu, tuangalie kipengele cha eneo la utafiti.

**Eneo la Utafiti**
Makala hii inalenga kubainisha vyanzo vya misimu kwa wanachuo wanaosoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mtafiti ameteua eneo hili akiamini kuwa chuoni hapo ndipo hasa atapata rika la vijana ambao ndiyo watumiaji wakubwa wa misimu ikilinganishwa na rika nyinginezo. Pia eneo hili ni chanzo muhimu cha data inayofanyiwa utafiti katika makala hii. Aidha, ni vigumu kwa mtafiti kukusanya data kutoka katika maeneo mengi kutokana na ufinyu wa muda na bajeti iliyopangwa kwa ajili ya kukamilisha zoezi hili. Halikadhalika, mtafiti amewiwa kubainisha misimu inayotumiwa na watafitiwa hawa ili ijulikane kwa wasanifishaji na wakuzaji wa lugha ya Kiswahili kama vile BAKITA na BAKIZA. Kipengele kinachofuata kinahusu misimu inayotumiwa na wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika nyanja za utani, soka na sanaa. Ufafanuzi unatolewa ili kuthibitisha kauli hiyo.

**Vyanzo vya Misimu Inayotumiwa na Wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**
Makala hii inachunguza vyanzo vya misimu mbalimbali inayotumiwa na wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Matokeo ya makala yanaonesha kuwa vipo vyanzo vya misimu kadhaa inayotumiwa na watafitiwa hao. Vyanzo hivyo vimeangaliwa kutokana na nyanja za utani, soka pamoja na sanaa. Tuangalie ufafanuzi ufuatao ili kuelewa zaidi.

**Misimu ya Utani**
Miongoni mwa vyanzo vya misimu kwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni pamoja na utani. Utani hutumika miongoni mwa wanajamii na hudumisha amani, upendo na mshikamano pale usipovuka mipaka. Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama walivyo wanachuo wa vyuo vingine ulimwenguni, nao hutaniana. Utani huu hautumii tu msamiati uliyosanifishwa bali pia hutumia msamiati usiyosanifishwa yaani misimu. Ifuatayo ni misimu inayotokana na utani*: GB*, *jishaua*, *karai*, *kiki*, *kimeumana*, *kitonga*, *kontena jipya*, *kuprinti*, *mburura*, *mwamba*, *nyodo*, *pamba kali*, *pepsi big, piga mbonji*, *pisi kali*, *sepa*, *September conference*, *shatopori*, *tangopori* na *zingua*. Data ya makala hii inaonesha kuwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hutaniana kwa kutumia msimu *GB* wakimaanisha makalio. Msimu huu hutumika miongoni mwa wanachuo hao kama sehemu ya kupunguza ukali wa neno makalio au matako, haijalishi ni makalio makubwa au madogo. Pia huutumia ili kufanya mazungumzo yao kuwa ya siri kwani ni vigumu mtu mwingine asiyekuwa mwanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutambua maana ya msimu huo. Aidha, msimu *jishaua* hutumiwa na wanachuo hao wakimtania mtu mwenye tabia za kujidai, kujigamba, kujiona mjuaji kuliko wengine na kadhalika. Hivyo, kama mtu ana tabia kama hizo utasikia wakisema fulani anajishaua. Watafitiwa wa makala hii pia hutumia msimu *karai* wakimtania mtu aliyepata daraja 'C' katika matokeo ya mitihani. Msimu huu waweza kutumika pale mwanachuo anapopata daraja 'C' katika somo moja au hata wakia kwa ujumla. Aidha, msimu *kiki* hutumika kuwatania watu wanaotafuta umaarufu kwa njia mbalimbali. Yaweza kuwa njia ya kujigamba, kujipendekeza na kadhalika. Hivyo, watu wa namna hii husemwa kuwa wanatafuta *kiki*. Mara nyingi watu hawa hupenda kujulikana na kuthaminiwa katika jamii.

Wanachuo hutumia msimu *kimeumana* wakimtania mtu aliyefikwa na kadhia au hali ya sintofahamu. Lakini pia huutumia msimu huu hata pale hali hii inapokuwa imewakumba wao kwa ujumla wao.

Kwa mfano, wakikuta mtihani umekuwa mgumu kwao, kupata alama chache kwenye jaribio, kazi za makundi, wakipewa adhabu fulani na kadhalika, hapo utasikia wakisema *kimeumana*. Msimu *kitonga* pia ni miongoni mwa misimu ya utani unaotumiwa na wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Msimu huu hutumika kuwatania wanachuo wanaopenda mambo ya mteremko au ya bure. Yaweza kuwa kupenda alama za bure, kuandikwa kwenye kazi za makundi wakati hawajashiriki kufanya kazi hizo, kutaka zawadi mbalimbali na kadhalika. Nao msimu *kontena jipya au toleo jipya*, ni msimu unaotokana na utani kwani hutumika kuwatania wanachuo wa mwaka wa kwanza pindi wanapowasili chuoni kwa mara ya kwanza. Hivyo, wanachuo ambao ni wazoefu huwatania wageni kwa kusema kuwa chuo kimemwaga *kontena jipya au toleo jipya*.

Aidha, msimu *kuprinti* ni mojawapo ya misimu unaotumiwa na wanachuo hawa wakiwatania wenzao wanaotembea kwa mguu. Dhana ikiwa ni kufananisha zile nyayo zinazobaki ardhini wakati mtu akitembea kwa mguu na wino unaojitokeza katika karatsi wakati wa kuprinti kazi fulani. Nao msimu *mburura* unatumika kuwatania wanachuo wenye uwezo mdogo wa kutambua na kuzingatia mambo mbalimbali. Yanaweza kuwa ya kielimu au ya kijamii. Pia wanachuo wanaopewa jina hili (mburura) huwa na uwezo mdogo wa kudadavua mambo ama ya kielimu au ya maisha kwa ujumla. Matokeo ya makala hii yanaonesha pia kuwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hutumia msimu *nyodo* kuwatania watu wenye tabia za kuringa, kujisikia au kujiona bora. Kupitia mbinu ya usaili, watafitiwa wa makala hii wamesema kuwa hutumia msimu *pamba kali* wakiwatania watu waliovaa nguo nzuri na za gharama. Pia imebainika kuwa wanachuo hawa huwatania wenzao kwa kutumia msimu *pepsi big*. Msimu huu hutumika kama jina kwa wanawake wenye maumbile makubwa. *Piga mbonji*. Huu ni msimu utumikao kuwatania wanachuo wanaopenda kulalalala au kupiga usingizi ilihali wenzao wanajishughulisha na masuala ya masomo.

Data ya makala hii inaonesha kuwa msimu *pisi kali* umeshika kasi katika chuo hiki. Watafitiwa wa makala hii hutumia msimu huu kama utani kwa wasichana warembo. *Shatopori* kwa mujibu wa watafitiwa, *shatopori* ni msimu unaotumika chuoni hapo ili kuwatania wale wanaopita njia za pembezoni pasipo kupanda shato (magari yanayowasafirisha wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutoka kwenye nyumba zao za kulala mathalani, hosteli kwenda chuoni na kuwatoa chuoni kuwarudisha hosteli).

**Misimu ya Soka**

Kwa mujibu wa data ya makala yetu, soka ni chanzo kizuri cha misimu kwa watafitiwa wa makala hii. Watafitiwa hawa hushabikia soka na hivyo hutumia misimu mingi inayohusiana na soka. Aidha, misimu inayotokana na uwanja huu hupendwa sana kwani kwao soka ni mojawapo ya kiburudisho. Ifuatayo ni misimu inayotokana na soka inayotumiwa na wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: *benchi la ufundi*, *kuupiga mwingi*, *makolo*, *mchongo*, *mpapaso*, *utopolo*, *wa hapahapa FC* na *wa kimataifa FC*. Msimu *Benchi la ufundi* katika soka hurejelea mjumuiko wa wataalamu wenye majukumu ya kufundisha na kuhudumia timu. Kwa mfano, kocha, madaktari, mtunza vifaa, meneja wa timu na kadhalika. Kutokana na maana ya msimu huu, wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamejiundia maana nyingine inayoendana na hiyo. Kwa mujibu wao, *benchi la ufundi* ni kikundi cha muda mfupi cha wanachuo kinachoundwa kwa ajili ya kujadiliana kuhusiana na masomo mbalimbali

kabla ya kuingia kwenye chumba cha mtihani. Hivyo, maana ya msimu huo katika soka imehusishwa na lile kundi la wanachuo linaloundwa kwa minajili ya kusaidiana kwa zoezi la mitihani linalowakabili. Kupitia mbinu ya usaili imedhihirika kuwa watafitiwa hutumia pia msimu *kuupiga mwingi* ulioibuka kutokana na soka. Katika soka, msimu huu humaanisha mchezaji kucheza vizuri sana. Mathalani, kupiga chenga, kukimbia, kufunga, kukaba ipasavyo, kupiga mpira kwa mwendo mrefu kwa mfano kutoka gori moja hadi jingine ama kutoka kwenye nusu ya uwanja hadi gorini na kadhalika. Tofauti na uwanja wa soka, msimu huu umehamia hata katika nyanja nyinginezo kama vile siasa, elimu, jamii maeneo mengine mengi. Maana inayotumika katika nyanja hizi ni mtu kufanya jambo fulani kwa ufanisi mkubwa. Kwa mfano, watafitiwa wa makala hii hutumia msimu huu kumsifia raisi wa Tanzania Mama Samia Suluu Hassan kuwa anaupiga mwingi. Maana yake anafanya mambo kadhaa kwa ufanisi kama vile ujenzi wa miundo mbinu, kuipa elimu kipaumbele, kupandisha mishahara na madaraja kwa watumishi na masuala kadhaa ya kijamii. Vilevile hutumia msimu huu kuwasifia watu wanaojituma katika kufanikisha mambo mbalimbali kiufanisi kama vile wanachuo wanaojitahidi kimasomo, wahadhiri wanaofundisha vizuri na masuala mengine mengi yanayotimizwa kwa ufanisi mkubwa. Soka pia imezalisha msimu *makolo*. Msimu huu umetokana na aliyekuwa msemaji wa timu ya simba Haji Manara ambaye kwa sasa ni msemaji wa timu ya Yanga.

Ni baada ya kuachana na timu ya simba na kuingia yanga akatumia nafasi hiyo kuwatania simba ya kuwa jezi zao zimejaa makolokolo kwa maana ya mapichapicha ya kila aina. Hii ilikuwa njia ya kuzisifia jezi za yanga kwamba hazina makolokolo kama yale ya jezi za simba. Basi msimu huu umeshika kasi miongoni mwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwani mashabiki wa timu ya yanga huutumia kuwatania mashabiki wa simba ambao ni watani wao. Msimu mwingine uliyoonekana kutokana na soka ni *mchongo*. Msimu huu unatokana na soka kupitia mchekeshaji wa lafudhi ya Kinyakyusa ajulikanaye kama 'Mwaisa Mtu Mbadi' pale alipokuwa akiwakosoa waamuzi wa mpira wa miguu akidai kuwa wameipatia timu ya yanga penati isiyokuwa ya halali. Hivyo, msimu huu umezagaa chuoni hapo na kupatiwa maana mpya. Maana iliyoibuka kutokana na msimu huu ni hali ya mtu kutaka kufanyiwa jambo au kupewa kitu kisicho cha halali, mathalani, alama za bure (alama za mchongo). Sambamba na misimu hiyo, upo msimu mwingine ujulikanao kama *mpapaso*. Msimu huu uliibuliwa na msemaji wa timu ya Mtibwa Sugar, Bw. Masau Bwire. Kwa mujibu wa TATAKI (2014) papasa ni tendo la kugusa kwa upole. Kutokana na fasili hii, msimu *papasa* umepewa maana tofauti kabisa, msemaji huyu alimaanisha timu yake kuwashinda wapinzani wanaokuwa wanakabiliana nao.

Matokeo ya makala hii yanaonesha pia kuwa soka limekuwa chanzo cha kuibuka kwa misimu kwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hii ni kutokana na msimu *utopolo* uliyoibuliwa na Haji Manara aliyekuwa msemaji wa timu ya simba ambaye amehamia timu ya yanga kwa sasa kama ilivyodadavuliwa hapo juu. Msemaji huyu huwatania wapinzani wake ambao ni yanga kwa kuwaita *utopolo* kabla ya kuhamia katika timu hiyo akitokea simba. Hivyo, mashabiki wa simba hapa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam huutumia msimu huu kuwatania wapinzani wao ambao ni mashabiki wa yanga kwa kutumia msimu huo. Halikadhalika, watafitiwa wamesema kuwa mashabiki wa timu ya simba hutuma msimu *wa hapahapa FC* kuwatania wapinzani wao ambao ni yanga. Maana ya msimu

huu kulingana na uwanja wa soka, ni kwamba timu ya yanga ni ya kushindania makombe ya humuhumu Tanzania na si nje ya hapo. Hii ni kutokana na timu hii kutokupata ushindi wa kushindania makombe ya kimataifa. *Wa kimataifa FC*. Huu ni msimu unaotumiwa na mashabiki wa timu ya simba katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakimaanisha kuwa wao ni viwango vya kimataifa japokuwa hawajawahi kuchukua kombe la kimataifa.

**Misimu ya Sanaa**

Mbali na chanzo cha utani na soka miongoni mwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vilivyodadavuliwa hapo juu, ipo pia misimu kadhaa inayotumiwa chuoni hapo ambayo chanzo chake ni sanaa. Tunaweza kusema kuwa sanaa ni ufundi unaotumiwa na watu katika kuwasilisha mawazo na fikra zao. Kupitia mbinu ya hojaji na usaili, watafitiwa wamethibitisha wazi kuwa sanaa imetoa mchango mkubwa katika suala zima la kukuza lugha ya Kiswahili kupitia misimu yake. Hii ni kutokana na sababu kuwa baadhi ya misimu ya sanaa imeenea maeneo mbalimbali nchini Tanzania, imeshika mizizi na kutumiwa na watu wengi katika jamii ya watanzania. Sababu ya misimu ya sanaa kuenea sehemu mbalimbali na kutumika kwa wingi ni kutokana na sababu kuwa sanaa inapendwa sana, na huwasilishwa kwa njia ya mitandao ya kijamii na vyombo vya habari. Ikimbukwe kuwa vyanzo hivi vina watumiaji wengi na vina nguvu kubwa ya kusambaza taarifa katika jamii kwa asilimia kubwa na kwa haraka sana. Hivyo, misimu ya sanaa husambaa haraka, hupendwa na hutumiwa na watu wengi katika jamii husika. Aidha, wasanii ni kioo cha jamii na ni ngao muhimu yenye dhima kadhaa katika jamii mathalan, kuonya, kuelimisha, kuwa mifano ya kuigwa na kuijenga jamii kwa ujumla. Matokeo ya data ya makala hii yanathibitisha kuwa misimu ya chanzo hiki ina athari kubwa na hutumiwa sana na wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ifuatayo ni misimu inayotokana na chanzo hicho cha sanaa: *chura*, *kulelewa*, *kwio*, *marioo*, *mchepuko*, *njia kuu*, *skendo*, na *software*. Kwa maelezo ya watafitiwa kupitia mbinu ya hojaji, ni kwamba msimu chura umetokana na msanii wa muziki wa kizazi kipya ajulikanaye kama Snura. Chura ni wadudu ambao baadhi yao huishi majini na baadhi nchi kavu. Msimu huu umepewa jina hilo kutokana na sababu kuwa wanenguaji wa msanii huyo hujilaza majini na kubinua makalio mithili ya umbile la chura. Hivyo, mtindo huo wa uchezaji ukapewa jina la wadudu hao.

Mbali na hilo, watafitiwa wameeleza pia kuwa msimu huu hutumika kwa wanawake wenye makalio makubwa. Msimu mwingine unaotumiwa na wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutokana na chanzo cha sanaa ni *kulelewa*. Chanzo cha msimu huu ni sanaa ambapo msanii ajulikanaye kama Marioo anautumia kuwaasa vijana wa kiume wanaopenda kutunzwa na wanawake wenye umri mkubwa zaidi yao. Hivyo, msimu huu humaanisha tendo la vijana au watoto wa kiume kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanawake watu wazima ili wapatiwe mahitaji yao ya kimaisha. Msimu *kwio* pia kutokana na matokeo ya data yetu umetokana na sanaa ambapo msimu huu ulitolewa na msanii Gig Man. Kama tulivyoelezea kuwa, wasanii na sanaa zao hupendwa sana katika jamii na hivyo kuipelekea jamii kuiga kila wafanyacho. Msimu huu hauna maana yoyote ile ila jamii wakiwemo wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hutumia msimu huu kwa sababu tu umetumiwa na msanii. Hali hii ilipelekea Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kuupiga marufuku. Kutokana na msanii Marioo kuwaasa vijana wasipende kulelewa, suala hilo liliwafanya vijana wa Chuo Kikuu

cha Dar es Salaam kuwapa jina la *Marioo* vijana wa kiume wenye tabia ya kupenda kulelewa. Hivyo, msimu *marioo* huwarejelea vijana wenye tabia tajwa hapo juu. Sambamba na misimu hiyo, pia msimu *mchepuko* na *baki njia kuu* umetokana na uwanja wa sanaa. Mwanzilishi wa misimu hii ni aliyekuwa mtangazaji wa Clouds FM Ephraim Kibonde (kwa sasa ni marehemu). Alitoa misimu hii katika tangazo lake lililokuwa na maudhui ya kuwaonya wanaume na wanawake wasiokuwa waaminifu katika ndoa zao. Hivyo, *mchepuko* unarejelea mke au mme anayemsaliti mwenzie kwa maana kuwa anaacha njia kuu ambayo ni ndoa na kuchepukia pembeni mwa njia hiyo (mchepuko ni yule anayesababisha hali hiyo ya kumsaliti mwanandoa). Watafitiwa wa makala hii kupitia mbinu ya usaili wamebainisha pia kuwa msimu *skendo* umetokana na sanaa. Hii imetokana na sababu kuwa wasanii wamekuwa na kasumba ya kukumbwa na matukio kadhaa katika maisha yao kila siku. Hasahasa msimu huu unahusishwa na msanii Wema Sepetu msanii wa Bongo Movi kutokana na kuwa na matukio ya hapa na pale. Hivyo, badala ya kusema fulani amekuwa na matukio mengi msimu *skendo* hutumika.

Tumeona misimu kadhaa iliyotokana na sanaa. Kwa hakika ni mingi na inatumika miongoni mwa wanachuo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Misimu mingine tuliyoibaini inayotokana na uwanja huu, ni kama vile: *software*. Kwa maelezo ya watafitiwa wa makala hii ni kwamba msimu huu umetokana na msanii wa vichekesho na muigizaji ajulikanaye kama Maufundi. Kwa maelezo ya msanii huyu ni kwamba *software* ni kufanya jambo lolote lile bila kutumia nguvu. Kwa maelezo ya watafitiwa ni kwamba hii ilitokana na swali aliloulizwa msanii Maufundi na waandishi wa habari kwamba, 'kuwachekesha watu ni shughuli pevu, je, wewe hutumii nguvu kushawishi watu ili wacheke?' Jibu lake lilikuwa kwamba, 'vichekesho ni kipaji changu. Hivyo, natumia *software* katika kuwachekesha watazamaji wangu.' Hii ina maana kuwa hatumii nguvu ili kuwachekesha watazamaji wake. Kwa ujumla, matokeo ya makala hii ni uthibitisho tosha kwamba wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hutumia misimu itokanayo na vyanzo vya utani, soka na sanaa. Kifuatacho ni kipengele cha hitimisho la makala yetu.

**Hitimisho**

Suala la kuibuka na kutumika kwa misimu haliepukiki katika jamii iwayo yoyote ile. Hii ni kutokana na sababu ya matukio mbalimbali na mambo kadhaa yanayohitaji maneno au msamiati unaoweza kukidhi haja ya mawasiliano miongoni mwa watumiaji wa lugha husika. Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hutumia misimu iliyotokana na vyanzo mbalimbali. Miongoni mwa vyanzo hivyo ni: utani, soka na sanaa. Misimu iliyotokana na utani ni: *GB*, *jishaua*, *karai*, *kiki*, *kimeumana*, *kitonga*, *kontena jipya*, *kuprinti*, *mburura*, *mwamba*, *nyodo*, *pamba kali*, *pepsi big*, *piga mbonji*, *pisi kali*, *sepa*, *September conference*, *shatopori*, *tangopori* na *zingua.* Kwa upande wa soka tumebaini misimu kama vile: *benchi la ufundi*, *kuupiga mwingi*, *makolo*, *mchongo*, *mpapaso*, *utopolo*, *wa hapahapa FC* na *wa kimataifa FC.* Pia data ya makala hii inaonesha kuwa chanzo cha sanaa kimekuwa na mchango katika kuzalisha misimu chuoni hapo. Ifuatayo ni misimu iliyotokana na chanzo cha sanaa: *chura*, *kulelewa*, *kwio*, *marioo*, *mchepuko*, *njia kuu*, *skendo*, na *software*. Makala hii ina umuhimu katika jamii kwani imekuwa chachu katika suala zima la kuangazia vyanzo vitatu vya misimu kwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama vilivyobainishwa hapo juu. Aidha, imetoa mchango kwa taasisi zinazohusika na usanifishaji wa lugha ya Kiswahili; BAKITA na BAKIZA

ili ziweze kuchambua misimu yenye mashiko na manufaa kwa jamii na kuisanifisha. Kwa vile utafiti huu umeshughulikia vyanzo vya misimu vya utani, soka na sanaa peke yake miongoni mwa wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, inapendekezwa kuwa utafiti mwingine ufanyike kuhusiana na vyanzo vingine vya misimu kama vile: maendeleo ya sayansi na teknolojia, mitandao ya kijamii, elimu, uchumi, jamii na kadhalika. Aidha, ufanyike utafiti kuhusiana na madhara yatokanayo na misimu lakini pia mchango wa misimu katika lugha mbalimbali.

## Marejeleo

Chacha, E. P. (2001) "The Use of Ethnic Community Languages in Urban Areas in Tanzania: A Case Study of Kikuria in Dar es Salaam." Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chapman, R. L. (1995). *Dictionary of American Slang*. New York: Haper Collins Publishers.

Fishman, J. A. (1972). "Domains and the Relationship between Micro- and Macro-Sociolinguistics." In Gumperz, J and Hymes, (eds.). *Directions in Sociolinguistics*. New York, Holt Rinehart and Winston, Inc. Ku. 435-453.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimu jamii.* Dar - es - Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. (2006) *Proposal and Thesis Writing*. Nairobi: Pauline Publications Africa.

Mekacha, R. D. K. (1993). "The Sociolinguistics Impact of Kiswahili on Ethnic Community Languages in Tanzania: A case study of Ekinata". Bayreuth African Studies.

Msanjila, Y. P. (1999). "The use of Kiswahili in Rural Areas and its Implications for the Future of Ethnic Languages in Tanzania". Ph.D Thesis, University of Dar es Salaam.

Msanjila, Y. P. (2009). *Isimu jamii Sekondari na Vyuo*. Dar - es - Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (1989). "Tanzu za fasihi simulizi". Mulika Juz 21, kur. 1- 24.

Mulokozi, K. (1999). "Tenzi Tatu za Kale". Dar es Salaam: TUKI.

Neuman, W. L. (1991). *Social Research Methods*. A Division of Simon and Schuster, Inc.

Shayo, I. (2015). "Semi zilizoandikwa katika Maeneo ya Biashara; Uchunguzi kuhusu Asili, Muundo, Miktadha, na Utokeaji na Dhima". Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

TATAKI. (2014). *Kamusi ya Kiingereza–Kiswahili Swahili–English Dictionary*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Focus Publications Limited.